## Azimio la Waislamu kuhusiana na Mabadiliko ya Tabia Nchi Ulimwenguni

*Kwa jina la Allah Mwingi wa Rehema na Mwenye Kurehemu*

**UTANGULIZI**

1.1 Mwenyezi Mungu - tunametambua kwa jina la Allah- ameumba ulimwengu wenye maumbile ya aina tofauti, yenye utajiri na umuhimu wa aina yake ikiwemo; nyota, jua na mwezi, sayari ya dunia na jamii ya viumbe vinavyoishi. Vyote hivi ni ushahidi wa neema zisizomithilika na rehema kwa muumba wake, na vyote vinanyenyekea kutokana na uwezo wa Bwana wake. Sisi wanadamu tumeumbwa kumuabudu Bwana wa viumbe wote, ikiwa ni kuwatendea wema viumbe wa aina zote kwa kadri tuwezavyo kuanzia sisi wenyewe na vizazi vijavyo ambavyo Mwenyezimungu ameviumba

1.2 Sayari yetu imeweza kuishi kwa mabilioni ya miaka na mabadiliko ya tabia ya nchi sio kitu kigeni. Tabia ya nchi duniani imekuwa ikibadilika kupitia awamu za vipindi vya mvua na jua; vipindi vya ubaridi na joto hii inatokana na mambo mengi ya maumbile asilia. Mengi ya mabadiliko haya yamekuwa yanatokea polepole kiasi ambacho jamii na mifumo ya kimaisha vimeweza kujirekebisha vyenyewe kuishi kuendana na hali hiyo. Kumekuwapo na mabadiliko tabia nchi yenye athari kubwa ambayo yamepelekea maafa makubwa, lakini haya hutokea kwa vipindi fulani tu ambapo badae hali za kimaisha hujirekebisha kutokana na athari hizo ambapo tena hujitokeza hali mpya inayoendana na mifumo ya kiekologia yenye uwiano kama vile ambavyo tunashuhudia hii sasa. Mabadliko ya tabia nchi katika nyakati zilizopita yalisababishwa na uwekaji kwa wingi wa mabaki ya nishati ambayo tunafaidika nayo. Pamoja na bahati tuliyokuwa nayo, matumizi yetu yasio ya busara na kutoona mbali katika matumnizi ya raslimali hizi imepelekea uharibifu wa hali halisi ambayo imewezesha uwepo wa maisha yetu katika sayari hii ya dunia.

1.3 Kasi ya mabadiliko ya tabia nchi iliopo hivi sasa inatofautiana kimpangilio kutokana na ukubwa wake kutoka mabadiliko ya pole pole ambayo yaliku yakitokea hapo kabla hadi kufikia zama hizi za karibuini. Haya yote, kwa kiasi kikubwa yamekuwa yakisababishwa na mwanadamu ambao tumekuwa wenye kuyatawalia maumbile kwa nguvu. Zama hizi tunazoishi zimeelezwa kwenye fani ya sayansi ya maumbile ya ulimwengu kuwa ni zenye kumhusu binadamu "zama za wanadamu".Pamoja na kuwa jamii yetu ya wanadamu, tumechaguliwa kuwa wachunga yaani *makhalifa* kwenye sayari hii ya ulimwengu hata hivyo tumekuwa sababu ya ufisadi na uharibifu wa ulimwengu huku tukijuwa kuwa tupo katika hatari ya kuangamiza maisha ya sayari yetu. Kiwango hichi cha mabadiliko ya tabia nchi hakiwezi kuachwa kiendelee, kwani huenda kipimo kizuri cha uwiano (*mizaan*) kilichowekewa dunia hii kitaweza kupotea mara moja. Kama tunavyojua, Binadamu tukiwa ni sehemu ya ulimwengu huu, jukumu letu kubwa ni kuyathamini mambile haya. Hata hivyo mabaki hayo hayo ya nishati ambayo inatusaidia kutimiza mahitajio yetu tunayoyaona leo hii, yamekuwa ndio sababu kuu ya mabadiliko ya tabia nchi. Uchafu mwingi unaotokana na mabaki ya nishati unatishia kuharibu zawadi tuliyoruzukiwa na Mwenyezimungu – Allah. Zawadi au neema hii ikiwemo hali ya hewa nzuri, hewa safi tunayoivuta, miongo mizuri ya hali ya hewa, na bahari zilizo salama. Lakini, tabia yetu kwa zawadi hii ni kuwa hatuiangalii vyema na tunaifanyia uharibifu. Je vizazi vijavyo

vitatuzungumzaje, ni nani atakaewachia wao urithi wa sayari hii iliyoyoharibika? Ni namna gani tutakabiliana na Mola wetu muumba wetu?

1.4 Tunanukuu katika ripoti tathmini ya karne kuhusu mfumo wa kiekologia wa ulimwengu iliyotolewa na Shirika la Kimazingira la umoja wa Mataifa (UNEP, 2005) na kupitishwa na wanasayansi 1300 kutoka nchi 95, ambapo imebainika kuwa "kiujumla, binadamu wamefanya mabadiliko makubwa ya mfumo wa kiekelogia katika kipindi cha nusu ya karne ya ishirini (20) kuliko muda wote uliopita katika historia ya mwanadamu. Pamoja na kuwa mabadiliko haya yamesaidia kuboresha maisha ya mwanadamu lakini vile vile yameambatana na ongezeko kubwa la uharibifu (wa mazingira yetu)."

> "Mwanadamu ndie anaesababisha athari hizo katika maumbile ya mifumo ya kiekologia ya sayari hii kiasi ambacho vizazi vinavyokuja havitaweza kufaidika."

1.5 Kukaribia miaka kumi inayokuja, pamoja na kuwepo mikutano mingi ya makubaliano juu ya maazimio ya Kyoyto, lakini kiujumla hali ya mazingira ya ulimwengu imezidi kuzorota. Katika ripoti ya utafiti wa mabadiliko ya tabia nchi ambayo ilitayarishwa na bodi inayojumuisha wajumbe wa serikali za mataifa mbali mbali yapatayo 100, ripoti hiyo iliyochapishwa mwezi Machi 2014, ilitoa sababu 5 zinazopasa kuzingatiwa ambazo kwa ufupi ni:

- Mifumo ya kiekologia na utamaduni wa mwanadamu tayari upo katika hatari itokanayo na mabadiliko ya tabia nchi
- Hatari zinazotokana na mabadiliko ya tabia nchi zinazosababishwa matukio makubwa kama vile mawimbi ya joto kubwa, mvua kubwa zisizo na mpangilio na ongezeko la mafuriko kwenye ukanda wa pwani hivi sasa zinaongezeka.
- Kiujumla hatari hizi hazipo sawa, ni kubwa sana kwa jamii masikini na zilizosahauliwa kwa kila nchi na katika ngazi zote za maendeleo.
- Athari zinazotabiriwa zitaathiri kwa kiasi kikubwa bio anuwai za ulimwenguni, raslimali na huduma zinazotokana na mifumo ya kiekologia pamoja na uchumi wa ulimwengu wetu.
- Msingi mkuu wa mifumo yenye kuonekana ya ulimwegu umo hatarini kuweza kupata mabadiliko ya ghafla na yasiyoweza kujirudi.

Kutokana na tahadhari hizi, tumelazimika kuhitimisha kwa kusema kuwa, tuanfanya makosa makubwa katika matumzi ya maliasili zetu - ikiwa ni msingi wa maisha yetu katika ulimwengu. Kunahitajika kufanyika mapitio ya haraka kutathmini hali ilivyo hivi sasa. Wanadamu hawawezi kuhimili kuona maendeleo ya kusuasua ya michakato inayoonekana katika mikutano yote ya nchi washirika wa makubaliano ya mabadiliko ya tabia nchi tangu wakati ilipotolewa ripoti ya mifumo ya kiekologia ya ulimwengu ya mwaka 2005, vile vile pamoja na misimamo iliopo hivi sasa.

1.6 Katika kipind kifupi tangu mapinduzi ya viwanda, wanadamu wameweza kutumia maliasili nyingi zisizorejesheka ambapo ulimwengu umechukuwa miaka 250 kuzizalisha- yote haya yanafanyika kwa kisingizio cha maendeleo ya kiuchumi na kibinadamu. Tunachukulia jambo hili kwa

tahadhari, athari ya ujumla ya kukua pato la mtu mmoja mmoja pamoja na kuongezeka kwa idadi ya watu. Halikadhalika tunachukulia hili tena kwa tahadhari kuwa mashindano ya kimataifa katika kuzidi kulimbikiza mabaki ya nishati ya mafuta kwenye vilele vya barafu vinavyoyeyuka katika maeneo ya aktiki

1.7 Wataalamu wanaoongoza masuala ya tabia nchi, hivi sasa wanaamini kuwa kuongezeka kwa joto la ulimwengu kwa nyuzi joto mbili, ambayo inazingatiwa kuwa "ni kiwango cha juu". Kwa hivi sasa yaweza kuwa kiwango hichi hakiwezi kuepukika ikiwa tutaendelea mtindo wetu wa kuona kila kitu ni cha kikawaida yetu tu. Hiki ni kiwango kinachozingatiwa kuwa ni kuingia katika janga kubwa la mabadiliko ya tabia nchi ambapo bado yatawafanya mamilioni ya watu na viumbe vyengine visivohesabika kukabiliwa na ukame, njaa na mafuriko. Athari ya yote haya itaendelea kuwakabili watu masikini, wakati dunia inashuhudia kuongezeka kukubwa kwa kiwango cha gesi ukaa kwenye anga inayozalishwa tokea yalipoanza mapinduzi ya viwanda

1.8 Ni jambo la kutisha kuona kuwa, pamoja na tahadhari na makadirio yote, mkutano uliofuata baada mkutano wa Kyoto uliotakikana kufanyika mwaka 2012 ulicheleweshwa kufanyika. Ni muhimu kuwa nchi zote hususan mataifa yaliyoendelea, kuongeza juhudi za kuunga mkono mchakato unaohitajika ili kuzuwia na kwa matumaini hatimaye kukabiliana na madhara ambayo tayari yananyemelea.

**TUNATHIBITISHA**

2.1 Tunathibitisha kuwa Allah ni Mola na Mlezi wa viumbe wengi

الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ

Shukrani zote zinamstakia MwenyeziMungu Mola wa walimwengu wote.

Qur'an 1: 1

هُوَ اللَّهُ الْخَالِقُ الْبَارِئُ الْمُصَوِّرُ

Yeye Allah – Muumbaji, mtengenezaji, mfanyaji wa sura (za namna kwa namna za viumbe)

Qur'an 59: 24

الَّذِي أَحْسَنَ كُلَّ شَيْءٍ خَلَقَهُ

Ambaye ametengeneza vizuri umbo la kila kitu.

Qur'an 32: 7

Hakuna ambacho kimeumbwa ambacho hakina faida; kila kitu kilichoumbwa kimeumbwa kwa makusudio maalum (kwa haqi)

وَمَا خَلَقْنَا السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَا لَاعِبِينَ مَا خَلَقْنَاهُمَا إِلَّا بِالْحَقِّ

Qur'an 44: 38

Na hatukuumba mbingu na ardhi na vilivyomo baina yake kwa ajili ya mchezo tu. Hatukuumba hivyo isipokuwa kwa haki.

2.2 Tunathibitrisha kuwa Allah amevizunguuka kuvijua vyote alivyoviumba

وَلِلَّهِ مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَمَا فِي الأَرْضِ وَكَانَ اللَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ مُّحِيطًا

Vinamthibitikia yeye vyote vilivyomo mbinguni na ardhini. Allah amevizunguuka kuvijua viitu vyote.

Qur'an 4: 125

Tunathibitisha kuwa:

- Mwenyezimungu ameumbia ulimwengu kwa kipimo maalum
- Kwa reheme yake kubwa tumepewa ardhi yenye rutba, hewa safi, maji safi na vitu vyote vizuri kwenye ulimwengu kwa ajili ya kuyafanya maisha yetu hapa yawe mazuri na yenye furaha.
- Harakati za Duniani katika mwenendo wa misimu asilia na mizunguuko yake; hali ya hewa ambayo viumbe hai wakiwemo wanadamu wanaendelea kuishi vizuri
- Majanga yanayotokana na mabadiliko ya tabia nchi hivi sasa ni matokeo ya mwanadamu kuharibu kipimo cha maumbile alichoweka muumba–

وَالسَّمَاء رَفَعَهَا وَوَضَعَ الْمِيزَانَ
أَلاَّ تَطْغَوْا فِي الْمِيزَانِ
وَأَقِيمُوا الْوَزْنَ بِالْقِسْطِ وَلا تُخْسِرُوا الْمِيزَانَ
وَالأَرْضَ وَضَعَهَا لِلأَنَامِ

Ameinua mbingu na ameweka kipimo. (mizaan)
Ili msiharibu kipimo hicho
Simamia katika kipimo kilichowekwa – Msichupe mipaka
Ameumba dunia kwa ajili ya viumbe vyote vinavyoishi

Qur'an 55: 7-10

2.3 Tunathibitisha ya kuwa Allah ameumba umbile asilia (*fitrah*)

فَأَقِمْ وَجْهَكَ لِلدِّينِ حَنِيفًا فِطْرَةَ اللَّهِ الَّتِي فَطَرَ النَّاسَ عَلَيْهَا
لا تَبْدِيلَ لِخَلْقِ اللَّهِ ذَلِكَ الدِّينُ الْقَيِّمُ وَلَكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لا يَعْلَمُونَ

Elekeza uso wake kuelekea kwenye umbile au mfumo asilia (halisi) ambao Allah ameuumba kwa watu

Hakuna mabadiliko kwa maumbile hayo ambayo Allah ameumba
Ni njia sahihi (asilia)
Lakini wengi hawaelewi

Quran 30: 30

2.5 Tunatambua kuwa ufisadi (uharibifu) ambao mwanadamu ameusababisha katika ulimwengu unatokana na kukosa subira katika kuendea ukuaji wa uchumi na matumizi yake. Athari za matokeo yake:

- Mabadiliko ya tabia nchi katika dunia ambacho ndio mazingatio yetu makubwa hiivi sasa, pamoja na hayo ni;
- Uchafuzi wa anga, ardhi, mifumo ya maji ardhini, na baharini kutokana na matumizi ya nishati.
- Kupotea kwa udongo,ukataji misitu ovyo na kuenea kwa jangwa
- Uharibifu, kutokomeza na kusambaratisha makazi ya viumbe vilivyopo ulimwenguni, maisha ya jamii na uharibifu wa aina mbali mbali ya mifumo ya kiuzalishaji na kibaolojia kama vile misitu yenye mvua, maeneo oevu ya maji baridi, na miamba matumbawe
- Kuharibiwa kwa faida na huduma zitokanazo za mifumo ya kiekolojia
- Kuingizwa kwa aina mbali mbali za kigeni na viumbe hai (wanyama na mimea) na kubadilisha geni zake au uasili wake.
- Kuathiri afya ya wanadamu ikiwemo kukaribisha maradhi mapya yanayojitokeza hivi sasa.

ظَهَرَ الْفَسَادُ فِي الْبَرِّ وَالْبَحْرِ بِمَا كَسَبَتْ أَيْدِي النَّاسِ لِيُذِيقَهُم بَعْضَ الَّذِي عَمِلُوا لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُونَ

Umedhihiri ufisadi katika bara na bahari kutokana na yale yaliyochumwa na mikono ya watu; ili Allah awape mtihani kutokana na baadhi ya yale waliyoyafanya, ili wapate kurejea kwa Allah

Qur’an 30: 41

Tunatambua kuwa sisi ni sehemu ya mpangilio uliotukuka, bado katika mpangilio huu ni viumbe wa pekee wenye nguvu na tuna jukumu la kutenda mema na kukataza mabaya kwa kila njia tunayoweza. Na vile vile tunatambua kuwa-

وَمَا مِن دَآبَّةٍ فِي الأَرْضِ وَلاَ طَائِرٍ يَطِيرُ بِجَنَاحَيْهِ إِلاَّ أُمَمٌ أَمْثَالُكُم

Na hakuna mnyama aliopo katika ardhi wala ndege arukaye kwa mbawa zake mbili
ila ni umati (jamii) kama nyinyi.
Qur’an 6: 38

- Sisi ni moja ua viumbe wengi wenye kuishi ambao tunaishi katika sayari hii na viumbe wengine
- Hatuna haki ya kuwakandamiza baki ya viumbe wengine au kuwasababishia madhara
- Hisia za kujua mema na mabaya inahitajika upande wetu, kama imani yetu inavyotuamrisha, kuwaangalia viumbe wote kwa uangalifu na kumuogopa muumba wetu, mwingi wa rehema na mwenye kututendea wema (ihsani) kwetu

لَخَلْقُ السَّمَاوَاتِ وَالأَرْضِ أَكْبَرُ مِنْ خَلْقِ النَّاسِ وَلَكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لا يَعْلَمُونَ

Qur'an 40: 57

Kwa yakini umbile la mbingu na ardhi ni kubwa kuliko umbile la wanadamu

1.7 Tunatambua kuwa sisi tutawajibika kwa matendo yetu yote

فَمَن يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ خَيْرًا يَرَهُ
وَمَن يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ شَرًّا يَرَهُ

Basi na anaefanya wema hata wa kiasi cha uzito wa mdudu chungu ataona jaza yake; na anaefanya uovu hata wa kiasi ya uzito wa mdudu chungu ataona jaza yake.

Qur'an 99:6-8

2.8 Kwa uoni wa mazingatio haya tunathibitisha kuwa majukumu yetu tukiwa waislamu ni kufata kiigizo cha mtume Muhammad (Rehema na Amani zimshukie juu yake -SAW) ambae:

- Ametangaza na kulinda haki za viumbe wote wenye kuishi. Kukataza utamaduni wa kuzika watoto wachanga wa kike wakiwa wazima, kupiga marufuku kuua viumbe hai kwa ajili ya michezo, aliewaelekeza masahaba wake matumizi mazuri ya maji hata kwa ajili ya kutawadha kwa kuswali. Alizuia kukata miti katika jangwa, akamwamuru mtu ambae amechukua watoto wa ndege kutoka kwenye kiota chao kuwarejesha kwa mama zao, na alipokuja kwa mtu aliewasha moto kwenye kichuguu cha wadudu alimwamuru kumwambia "zima, zima"
- Alieweka maeneo matukufu (Harams) viunga vya Makka na Madina, ambapo miti asili imekatazwa kukatwa au kuangushwa na wanyama pori hawastahiki kuwindwa au kufanyiwa usumbufu.
- Aliweka maeneo ya uhifadhi (himas) kwa ajili ya matumizi endelevu ikiwemo maeneo ya malisho, uoto asili na wanyamapori.
- Aliishi maisha ya tahadhari kuepukana na matumizi ya kupita kiasi, upotevu na ya kujionesha (ria)
- Aliamuru kubadilisha matumizi au kutumia tena vitu ambavyo havikuweza kutosheleza kwa kutengeneza tena au kuwachilia mbali

- Kula chakula chepesi, chenye afya, ambacho kwa baadhi ya muda unachanganya matumizi ya nyama
- Onyesha shukrani kwenye maumbile ya ulimwengu
- Kama Ilivyobainishwa ndani ya Quran , Ni rehma kwa viumbe wote

**TUNATOA WITO**

3.1 Tunatoa wito kwa mkutano wa washiriki kwenye mkutano wa umoja wa mataifa wa mikakati ya mabadiliko ya tabia nchi na mkutano wa nchi washiriki wa protkali ya Kyoto unaofanyika mwezi Disemba mwaka huu wa 2015 kujadiliana jambo hili na kufikia hitimisho la makubaliano yenye uwiano kwa kuzingatia

- Maafikiano ya kisayansi kuhusiana na mabadiliko ya tabia nchi, ambayo ni kurekebisha uwepo wa kiwango cha gesi ukaa katika anga kiasi ambacho kitazuia kiwango cha muingiliano wenye kuleta madhara kwa wanadamu na mifumo ya kimazingira
- Hitajio la kuweka malengo yalio wazi na mifumo ya ufuatiliaji
- Madhara makubwa kwa dunia yetu hii kama tutashindwa kufanya hivyo;
- Dhamana kubwa ambapo mikutano ya washiriki inatakiwa ichuklue kwa niaba ya baki ya wanadamu ikiwemo kuutuongoza sisi katika njia mpya inayohusu dunia hii ya Allah.
- 

3.2 Hasa hasa tunatoa wito kwa mataifa tajiri na yale yanayozalisha mafuta kwa wingi

- Kuongoza njia kuondokana uzalishaji wao wa gesi chafu (ukaa) kwa haraka iwezekanavyo na si zaidi ya kati kati ya karne hii.
- Kutoa misaada ya kifedha na kiufundi kwa nchi masikini ili kufikia namna ya uondoaji wa gesi ukaa haraka iwezekanavyo
- Kutambua jukumu la kimaadili ili kupunguza matumizi kwa kiasi ambacho watu masikini wataweza kufaidika kutokana na kile kilichobaki katika maliasili zisizorejesheka za dunia hii
- Kuishi katika kiwango cha nyuzi joto 2 au hitaji la nyuzi joto 1.5 kwa mazingatio kwamba thuluthi mbili ya mabaki ya nishati katika sayari ya ulimwengu imebaki ardhini
- Kufikiria tena mazingatio ya faida isiyojali maadili yatokanayo na mazingira kwendea utunzaji wake na kuinua hali ya watu masikini duniani
- Kuwekeza katika uwekezaji wa uchumi wa kijani –wenye kuzingatia mazingira silia

3.3 Tunatoa wito kwa watu wa mataifa yote pamoja na viongozi wao -

- Wakusudie kuondosha uzalishaji wa gesi chafu (ukaa) haraka iwezekanavyo ili kuweza kumudu kumudu uwepo wa kiwango kinachotakiwa katika anga.
- Kujitolea kwa nafsi yao kwa asilimia 100% kutoka kwenye matumizi ya nishati zinazorejesheka au kuweka mkakati wa kiwango zero cha upunguzaji uzalishaji wa gesi ukaa haraka iwezekanavyo, kuondosha athari za kimazingira zitokanazo na shughuli zao

- Kuwekeza kiukamilifu kwenye nishati yenye kurejesheka, ambayo ni njia bora ya kupunguza umaskini na kufikia maendeleo endelevu;
- Kutambua kuwa kuukimbilia uchumi unaojitosheleza katika sayari iliyofungika ambayo tayari imediziwa kupita kiasi chake sio jambo linalowezekana. Ukuaji lazima uhamasishwe kwa njia ya busara na kwa kiasi maalum, kuweka kipau mbele kukuza uhimili wa mambo yote, na hasa yaliyo rahisi kujitokeza kutokana na athari za mabadiliko ya tabia nchi ambayo tayari yapo na yanatarajiwa kuendele kwa miaka mingi ijayo
- Kuweka mwendelezo wa mfumo mzuri wa kibinadamu kwa kuzingatia mbadala wa mfumo wa sasa wa kiuchumi unaomaliza rasilimali, kuharibu mazingira, na kuzorotesha usawa
- Kuzipa kipau mbele juhudi za kukabiliana (na mabadiliko ya tabia nchi) ikiwa ni pamoja na kutoa msaada sahihi kwa nchi ambazo wanaishi makundi ya watu walio katika mazingira magumu (ya chini) na uwezo mdogo wa kukabiliana (na matokeo ya mabadiliko ya tabia nchi) , na kwa makundi ya wanyonge, ikiwa ni pamoja na wenyeji wa asili, wanawake na watoto.

3.4 Tunatoa wito kwa washirika, taasisi za kifedha, na sekta ya biashara kuwa -

- Kuzingatia vyema kwenye matokeo ya shughuli zao za kiuchumi, na kuangalia kwa makini jukumu la kupunguza athari za uzalishaji ukaa na athari nyenginezo kwenye mazingira ya asili;
- Ili kupunguza athari za kimazingira kwenye shughuli zao, inapasa kujitolea kwa asilimia 100% kusaidia uwepo wa nishati zinazorejesheka (mbadala) na / au kuwa na mkakati uzalishaji sifuri (asilimia 0% ) mapema iwezekanavyo na kuhamia kwenye uwekezaji wa nishati mbadala;
- Kubadilika kutoka mfumo wa sasa wa biashara ambao unategemea misingi ya uchumi unaokua ambao usio endelevu na kujiweka kwenye uchumi mzunguuko ambao ni endelevu kiujumla;
- Kuweka mazingatio zaidi kwenye majukumu ya kijamii na kimazingira, hasa kwa kiasi kwamba wataweza kutafuta na kutumia rasilimali zilizo chache;
- Kusaidia katika kuzuia uwekezaji unaotegemea uchumi unaotokana na nishati ya mafuta na kutanua wigo kwendea matumizi ya nishati zinazorejesheka na njia nyengine mbadala zenye kuzingatia mazingira.

3.5 Tunatoa wito kwa makundi yote kuungana nasi, kushirikiana, ushirikiano na urafiki wemye ushindani katika jitihada hizi na tunakaribisha mchango mkubwa uliotolewa na imani za dini nyingine, kama tunavyoweza kusema kuwa sisi wote ni washindi katika ushindani huu

وَلَكِن لِّيَبْلُوَكُمْ فِي مَا آتَاكُم فَاسْتَبِقُوا الْخَيْرَاتِ

......Lakini (Allah) anataka kukujaribuni kwa yale aliyokupeni. Basi shindaneni kuyafikia mambo ya kheri

Qur'an 5: 48

Ikiwa kila mmoja angeweza kudumisha vizuri utamaduni wake, basi tungeona njia ya kuyatatua matatizo yetu

3.6 Mwisho, tunawaomba Waislam popote walipo ikiwemo:

- Viongozi wa kitaifa
- Viongozi wa kisiasa
- Jamii ya wafanyabishara
- Wajumbe wa mkutano wa Umoja wa mataifa kuhusiana na mabadiliko ya tabia nchi
- Viongozi wa dini na wanzuoni
- Mikusanyiko katika misikiti
- Taasisi za wakf za kiislamu
- Wasomi na taasisi za kielimu
- Viongozi wa kijamii
- Taasisi za kiraia
- Jumuiya zisizo za kiserikali
- Vyombo vya habari na mawasiliano

Kubadilisha tabia, akili, na sababu za msingi zinzosababisha mabadiliko ya tabia nchi, uharibifu wa mazingira na upotevu wa bayoanuwai katika maeneo ambayo walipo, kwa kufata mfano wa mtume Muhammad (SAW), na kuleta azimio kwa changamoto ambazo hivi sasa. Allah amesema katika Quran

وَلاَ تَمْشِ فِي الأَرْضِ مَرَحًا إِنَّكَ لَن تَخْرِقَ الأَرْضَ وَلَن تَبْلُغَ الْجِبَالَ طُولاً

Wala usitembee katika ardhi kwa maringo. Hakika wewe huwezi kuipasua ardhi wala kufikia urefu wa milima

Qur'an 17: 37

Tunayazingatia maneno ya Mtume (Rehema na Amani zimshukie juu yake -SAW)
Dunia ni njema na ya yenye kijani kibichi, na kwa hakika amekufanya msimamizi wa hiyo, na mnaangaliwa namna mnavyojitakasa.
(Hadithi iliyotajwa na Muslim kutoka kwa Abu Saʽīd Al-Khudrī)